Swali: Je Neno “Kalvari” tunalisoma wapi katika biblia?, na tofauti yake na Golgotha ni ipi?

JIbu: Katika biblia ya Kiswahili hakuna neno “Kalvari”, bali kuna neno “Golgotha” ambalo tunalisoma katika kitabu cha *Yohana 19:17*

> *Yohana 19:17 “Akatoka, hali akijichukulia msalaba wake, mpaka mahali paitwapo Fuvu la Kichwa, au kwa Kiebrania, GOLGOTHA.*
>
> *18 Wakamsulibisha huko, na wengine wawili pamoja naye, mmoja huku na mmoja huku, na Yesu katikati”.*

Maana ya Neno “Golgotha”, tayari biblia imeshatoa tafsiri yake hapo kwenye *mstari wa 17* kuwa ni *“Fuvu la Kichwa”*

Sasa neno “Kalvari” maana yake ni nini?

Neno Kalvari linapatikana katika tafsiri chache za lugha ya kiingereza, ambalo asili yake ni lugha ya Kilatini “CALVARIAE” lenye maana ile ile ya “Fuvu la kichwa cha mtu”.

Hivyo “Kalvari” na “Golgotha” ni Neno moja lenye maana moja, isipokuwa lugha tofauti, ni sawa na neno “church” na “kanisa” ni kitu kimoja ila lugha tofauti.

Kufahamu kwa upana ufunuo uliopo nyuma ya Golgotha, *(Fuvu la kichwa),* basi fungua hapa >>>FUVU LA KICHWA.[1]

Bwana akubariki.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kubofya link
hii >> https://chat.whatsapp.com/L3ysoFZcz058XCX9oLvKL1?s=cl&p=a&mlu=4&ilr=4[2]

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:
Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au

Piga namba hizi: +255789001312 au +255693036618

Mafundisho mengine:

KWANINI NDOA NYINGI ZINAVUNJIKA? (Sehemu ya 1: Upande wa wanaume)[3]

Je kunena kwa Lugha mpya kukoje?[4]

AMELAANIWA AANGIKWAYE MSALABANI.[5]

ALIFANYIKA SADAKA KWA AJILI YETU![6]

Biblia inaposema Yesu ameketi mkono wa kuume inamaana gani?[7]

Rudi nyumbani[8]

Share on:
WhatsApp

Endnotes:

1. FUVU LA KICHWA.: https://wingulamashahidi.org/2018/07/17/fuvu-la-kichwa/
2. https://chat.whatsapp.com/L3ysoFZcz058XCX9oLvKL1?s=cl&p=a&mlu=4&ilr=4: https://chat.whatsapp.com/L3ysoFZcz058XCX9oLvKL1?s=cl&p=a&mlu=4&ilr=4

3. KWANINI NDOA NYINGI ZINAVUNJIKA? (Sehemu ya 1: Upande wa wanaume): https://wingulamashahidi.org/2021/10/25/kwanini-ndoa-nyingi-zinavunjika-sehemu-ya-1-upande-wa-wanaume/
4. Je kunena kwa Lugha mpya kukoje?: https://wingulamashahidi.org/2019/09/02/je-kunena-kwa-lugha-mpya-kukoje-na-hizi-lugha-ni-zipi-na-je-ni-lazima-kila-mkristo-aliyepokea-roho-mtakatifu-anene-kwa-lugha-mpya/
5. AMELAANIWA AANGIKWAYE MSALABANI.: https://wingulamashahidi.org/2020/08/15/amelaaniwa-aangikwaye-msalabani/
6. ALIFANYIKA SADAKA KWA AJILI YETU!: https://wingulamashahidi.org/2019/08/12/alifanyika-sadaka-kwa-ajili-yetu/
7. Biblia inaposema Yesu ameketi mkono wa kuume inamaana gani?: https://wingulamashahidi.org/2023/12/02/biblia-inaposema-yesu-ameketi-mkono-wa-kuume-inamaana-gani/
8. Rudi nyumbani: https://wingulamashahidi.org